

# HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Jiji)

Simu Mkurugenzi : 255(28) 2501375  
Ofisi zote : 255 (28) 40334  
Fax : 255 (28) 2500785  
E-mail. [cd@mwanzacc.go.tz](mailto:cd@mwanzacc.go.tz)  
[info@mwanzacc.go.tz](mailto:info@mwanzacc.go.tz)



S. L.P. 1333  
**MWANZA.**  
**TANZANIA**

Kumb Na. E.30/1/Vol. IX/ 21

3 Novemba, 2017

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MSIMAMIZI WA KITUO**

1. Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la **Nyamagana** anatangaza nafasi za kazi ya **MSIMAMIZI WA KITUO CHA KUPIGIA KURA** ambaye atakuwa na jukumu la kusimamia shughuli za uchaguzi na kuhakikisha utulivu na usalama katika kituo cha kupigia kura kwenye Uchaguzi wa Marudio Kata ya Mhandu kujaza nafasi Wazi ya Diwani utakaofanyika **tarehe 26 Novemba, 2017.**

Aidha, majukumu mengine ya **Msimamizi wa Kituo** ni:-

- Kupokea na kutunza vifaa kwa ajili ya Uchaguzi katika kituo,
- Kuandaa na kufungua Kituo cha kupigia kura,
- Kutoa Karatasi za Kura kwa Mpiga Kura baada ya kuzigonga Mhuri wa Kituo,
- Kutoa ushauri na/au maelekezo kwa Wapiga Kura pale ambapo inahitajika kufanya hivyo,
- Kufunga Kituo mara baada ya saa za kufunga Kituo kutimia,
- Kuhesabu kura,
- Kuhakikisha kuwa Mawakala waliopo kituoni wanapewa fursa ya kujaza fomu zote zinzohusika,
- Kuandaa taarifa ya matokeo ya Uchaguzi ya Kituo na kuyabandika mahala pa wazi Kituoni, na kuwapatia nakala Mawakala walioshuhudia Matokeo ya Kituo hicho,
- Kushughulikia Malalamiko yanayojitokeza Kituoni na kukamilisha fomu zote za Malalamiko,
- Kukabidhi kwa Msimamizi/Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi masanduku yote ya kura, fomu za matokeo ya Uchaguzi na vifaa vyote vya Uchaguzi vilivyokabidhiwa kwake kwa ajili ya Kituo,

- Kuhakikisha kwamba Watendaji wa Kituo wote waliopo chini yake wanafahamu majukumu yao na kwamba atahakikisha anaweka utaratibu mzuri wa kujipanga katika utekelezaji wa majukumu ya kituo.

## **2. SIFA ZA MSIMAMIZI WA KITUO CHA KUPIGIA KURA**

- Awe raia wa Tanzania,
- Ikiwezekana* awe mkazi wa Kata ya MHANDU ambayo atafanyia kazi ya kusimamia Upigaji Kura na Kuhesabu Kura,
- Asiwe Kiongozi au Shabiki wa Chama cha Siasa,
- Awe *Mwadilifu, Mvumilivu, Mpole, Mtiifu, Msikivu* na anayeweza *kufanya kazi kwa kujituma*,
- Awe na elimu ya Kidato cha nne au zaidi na anayeweza kusoma na kuandika vizuri. Pia *anayeweza kuyaelewa Maelekezo ya Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura*,
- Awe na uwezo wa kuelewa vizuri Maelekezo ya Tume yanayohusu Orodha ya Wapiga kura,

## **3. UTARATIBU WA KUOMBA NAFASI YA KAZI**

Mwombaji anapaswa kuomba nafasi husika akitoa taarifa kamili zinazomhusu kulingana na sifa zilizotajwa na pia akitaja; kazi yake anayofanya hivi sasa, namba yake ya simu, Jimbo, na Kata anayokaa.

Aidha, ataambatanisha picha moja ya rangi yenye ukubwa wa pasi ya kusafiria (passport size), vyeti na kitambulisho chochote alichonacho.

Waombaji walioajiriwa wapitishie maombi yao kwa Waajiri wao.

Maombi yote yatumwe kwa:-

**Msimamizi wa Uchaguzi,**

**Jimbo la Nyamagana,**

**S.L.P. 1333**

**MWANZA**

Maombi ya nafasi ya kazi hii ya Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura yanaweza kuwasilishwa moja kwa moja

katika Ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi, Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

**4. MUDA WA MWISHO WA KUWASILISHA MAOMBI  
(DEAD LINE)**

Muda wa mwisho wa kuwasilisha Maombi ya nafasi ya kazi ni tarehe 11/11/2017 saa 9:30 Alasiri.

*KIOMONI KIBURWA KIBAMBA*  
**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**  
**JIMBO LA NYAMAGANA**